**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

**(OTM)**

# TAARIFA YA MATUKIO YA UINGIZAJI WA MIFUGO KWENYE HIFADHI KWA MWEZI NOVEMBA, DISEMBA, 2022, JANUARI NA FEBRUARI 2023 NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA

**Februari, 2023**

# YALIYOMO

1. UTANGULIZI ........................................................ 1

2. MATUKIO YA UINGIZWAJI WA MIFUGO HIFADHINI ........................................................ 4

2.1.Mkoa wa Mbeya ........................................................ 6

2.2.Mkoa wa Morogoro ........................................................ 15

2.3.Mkoa wa Katavi ........................................................ 17

2.4.Mkoa wa Mara ........................................................ 21

2.5.Mkoa wa Pwani ........................................................ 26

2.6.Mkoa wa Manyara ........................................................ 27

2.7.Mkoa wa Tabora ........................................................ 29

2.8.Mkoa wa Simiyu ........................................................ 29

3. UTARATIBU WA UKAMATAJI NA MAUZO... 32

3.1.Taratibu za Ukamataji ........................................................ 32

3.2.Taratibu za Mauzo ........................................................ 33

4. MAFANIKIO ........................................................ 34

5. CHANGAMOTO. ........................................................ 35

6. MAPENDEKEZO ........................................................ 37

7. HITIMISHO ........................................................ 39

# 1. UTANGULIZI

Makosa ya uingizaji wa mifugo hifadhini yamekuwa yakijirudia mara kwa mara. Kufuatia kukithiri kwa matukio hayo, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (OTM) iliweka utaratibu wa kukabiliana na changamoto hiyo kwa kuwafikishwa mahakamani watuhumiwa na kuwashtaki kwa makosa ya kuingiza mifugo hifadhini. Aidha, moja ya amri zilizoombwa mahakamani ni kutaifisha mifugo hiyo kwa mujibu wa Sheria ya Hifadhi Sura 282 na Sheria ya Uhifadhi wa Mazingira Sheria Na. 20 ya Mwaka 2004.

Hatua ya kuwafikisha mahakamani watuhumiwa imechukuliwa baada ya hatua za awali zilizochukuliwa na Mamlaka za Uhifadhi kuwa na changamoto nyingi katika utekelezaji wake. Changamoto hizo ni pamoja na;

i. Kwa mujibu wa Sheria, Mamlaka za Uhifadhi zimepewa uwezo wa kufifirisha makosa *(Compounding of Offences)*. Hata hivyo, hatua za ufifirishaji zilishindwa kuthibiti uhalifu katika hifadhi kwani licha ya wafugaji kupewa adhabu hiyo, wafugaji walewale waliendelea kuingiza mifugo hifadhini kwa idadi

kubwa zaidi ya mifugo. Kuendelea kuingia kwa mifugo hifadhini kunasababisha athari kubwa za ekolojia ya wanyama na uharibifu wa mazingira;

ii. Wamiliki wa mifugo kutelekeza mifugo yao hifadhini pindi tuu mifugo hiyo ikikamatwa, na wamiliki kutopatikana kwa wakati huku mamlaka za hifadhi zikiingizwa katika gharama za kutunza na kuhifadhi mifugo katika mazingira magumu;

iii. Ukosefu wa ulinganifu na uwiano wa kiasi cha pesa kinachotozwa wakati wa ufifirishaji;

iv. Kuwepo kwa tafsiri tofauti katika vifungu vya sheria vinahusiana na ufifirishaji kama ifuatavyo;

a) Sheria ya Hifadhi, Sura 282, ina vifungu viwili vinavyokinzana katika ukomo wa kiasi cha fecha kinachopaswa kutozwa. Wakati kifungu cha 20A(1)(i) Cha Sheria hiyo kinatoa ukomo wa kiasi kisichozidi Shillingi Laki Moja kutozwa pale ambapo mifugo itaingia hifadhini na kifungu cha

28(1)(a) kinatoa ukomo wa kiasi cha fedha kisichozidi Shillingi Laki Mbili pale mifugo itakapoingia hifadhini; na

b) Mbali ya vifungu vya 20A(1)(i) na 28(1)(i) kukinzana katika adhabu, lakini adhabu hii haijafafanua kama adhabu hiyo inayotajwa katika vifungo hivyo ni kwa kila mfugo unaoingizwa hifadhini ama ni kwa kundi la mifugo lililongia hifadhini pasipo kujali uwingi wake au umiliki wake.

v. Kuwepo na malalamiko mengi kutoka kwa wafugaji wanaodaiwa kupewa adhabu ya kufifirisha makosa ya kuingiza mifugo hifadhini bila kufuata sheria; na

vi. Zoezi la kufifirisha makosa ya kuingiza mifugo hifadhini limekuwa na malalamiko ya rushwa kwenye baadhi ya maeneo.

Kutokana na changamoto hizi, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilifanya maamuzi ya kufungua kesi mahakamani kwa kila tukio la mifugo kuingizwa hifadhini ili haki iweze kutendeka na kuonekana inatendeka na kuondoa dosari zilizokuwepo tajwa hapo juu.

## 2. MATUKIO YA UINGIZWAJI WA MIFUGO HIFADHINI

Katika miezi ya Novemba, Disemba 2022 hadi Januari, Februari 2023, jumla ya matukio **Thelathini na Nane (38)** ya mifugo kuingizwa hifadhini yaliripotiwa. Matukio hayo yalihusisha **ngo'mbe 5,583, punda 6 mbuzi 17 na kondoo 59** ambao waliingizwa katika Hifadhi za Taifa za Ruaha, Serengeti, Mwalimu Nyerere, Katavi, Kigosi na Tarangire. Jumla ya mashauri ya maombi **Thelathini na Nane (38)** yalisajiliwa mahakamani. Katika mashauri 37**,** Mahakama zilitoa amri ya utaifishaji *(consfiscation orders)* mifugo na katika Shauri mmoja (1) Mahakama ilitoa amri ya ufifirishaji (*compounding of offences).*

Kwa mashauri 37 ambayo amri ya utaifishaji ilitolewa, mifugo iliuzwa chini ya usimamizi wa Madalali wa Mahakama kwa mnada wa hadhara, ambapo kiasi cha Shillingi **Billioni Moja Millioni Mia Nne na Nane na Elfu Mbili Mia Nne (1,408,002,400.00)** zilipatikana. Katika shauri moja (1) ambapo mahakama ilitoa amri ya ufifishaji kiasi shilingi Millioni Ishirini na Nane

**(28,000,0000.00)** zilipatikana. Na hivyo kufanya jumla ya kiasi chote kilichopatikana kuwa shillingi **Billioni Moja Millioni Mia Nne na Thelathini na Sita na Elfu Mbili na Mia nne** (**1,436,002,400.00)**. Matukio hayo yalitokea katika Mikoa ya Mbeya, Katavi, Mara, Manyara, Pwani, Morogoro, Simiyu na Tabora.

## 2.1. Mkoa wa Mbeya

Katika Mkoa wa Mbeya, jumla ya matukio kumi na nne **(14)** ya uingiaji wa ng'ombe hifadhini yaliripotiwa yaliyohusisha ng'ombe **1,219.** Mashauri **14** yalifunguliwa Mahakama ya Wilaya Mbarali ya kuomba utaifishaji wa ng'ombe ambapo katika mashauri **13,** Mahakama ilitoa amri ya utaifishaji wa ngo'mbe **1,219** ambazo ziliuzwa na kiasi cha **Shiilingi 378,197,000.00** kilipatikana. Katika tukio moja lililohusisha ng'ombe **280** Mahakama ilielekeza Mamlaka zinazohusika kufanya ufifirishaji wa makosa. Kiasi cha **Shilingi 28,000,000.00** zilipatikana kutokana na ufifirishaji uliofanyika.

Matukio ya uingizaji wa mifugo hifadhini yalitokea katika Hifadhi ya Ruaha Wilayani Mbarali kwa nyakati tofauti kama ifuatavyo;

i. Tarehe 8/11/2022, ng'ombe **57** walikutwa katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha katika eneo la Kidimbwi, wamiliki wa ng'ombe hawakupatikana. Shauri Namba **13/2022** la Utaifishaji wa Ng'ombe lilifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya Mbarali. Mahakama ilitoa amri ya utaifishaji wa ng'ombe hao. Aidha, Mahakama ilitoa

amri ya ng’ombe hao kuuzwa kwa Mnada na Dalali wa Mahakama. Kiasi cha **Shillingi 18,090,000** kilipatikana. Katika mnada huu wastani wa ng’ombe mmoja aliuzwa kwa shillingi **317,368.42**;

ii. Tarehe 8/11/2022, ng’ombe **375** walikutwa katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha katika eneo la Mbuyuni, wamiliki wa ng’ombe hawakupatikana. Shauri Namba **14/2022** lilifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya Mbarali. Baada ya Shauri hilo kusikilizwa, Mahakama ilitoa amri ya utaifishaji wa ng’ombe hao, mnada uliendeshwa na Dalali wa Mahakama ambapo kiasi cha **Shillingi 76,526,000** kilipatikana. Ng’ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 204,069.33;**

iii. Tarehe 22/11/2022, ng’ombe **172** walikutwa katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha katika eneo la Mbuyuni, wamiliki wa ng’ombe hawakupatikana. Shauri Namba **17/2022** lilifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya Mbarali ambapo Mahakama ilitoa amri ya utaifishaji wa

ng’ombe hao, mnada uliendeshwa na Dalali aliyeteuliwa na Mahakama, kiasi cha **Shillingi 68,365,000** kilipatikana. Ng’ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 397,470.93;**

iv. Tarehe 25/11/2022, ng’ombe **10** walikamatwa katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha katika eneo la Ukangi. Katika tukio hili wamiliki wa ng’ombe hawakupatikana hivyo ililazimu Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kufungua Shauri Namba **19/2022** katika Mahakama ya Wilaya Mbarali. Baada ya Shauri hili kusikilizwa, Mahakama ilitoa amri ya utaifishaji wa ng’ombe hao, mnada uliendeshwa na Dalali wa Mahakama na kiasi cha **Shillingi 2,200,000** kilipatikana. Ng’ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 220,000.00**;

v. Tarehe 27/11/2022, ng’ombe **93** walikutwa katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha katika eneo la Ukangi. Wamiliki wa ng’ombe hawakupatikana. Shauri Namba **20/2022** lilifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya Mbarali na

Mahakama kutoa amri ya utaifishaji wa ng'ombe hao. Mnada uliendeshwa na Dalali wa Mahakama, kiasi cha **Shillingi 21,485,000** kilipatikana. Ng'ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 231,032.25**;

vi. Tarehe 27/11/2022, ng'ombe **13** walikutwa katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha katika eneo la Ikoga, wamiliki wa ng'ombe katika tukio hili hawakupatikana, hivyo, Shauri Namba **21/22** lilifunguliwa mahakamani katika Wilaya ya Mbarali. Mahakama ya Wilaya Mbarali ilitoa amri ya utaifishaji wa ng'ombe hao. Ng'ombe waliuzwa kwa mnada wa hadhara ulioendeshwa na Dalali wa Mahakama, kiasi cha **Shillingi 4,170,000** kilipatikana. Katika mnada huo, ng'ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 320.769.23**;

vii. Tarehe 27/11/2022, ng'ombe **280** walikutwa katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha katika eneo la Ukangi wamiliki wa ng'ombe hawakupatikana. Shauri Namba **22/2022** lilifunguliwa katika Mahakama

ya Wilaya Mbarali, wakati wa shauri likiwa Mahakamani wamiliki walijitokeza na Mahakama ilitoa amri ya Ufifirishaji ambapo kiasi cha **Shillingi 28,000,000** kilipatikana;

viii. Tarehe 13/12/2022, ng'ombe **38** walikutwa katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha katika eneo la Ukangi, wamiliki wa ng'ombe hawakupatikana. Shauri Namba **23/22** lilifunguliwa Mahakamani. Baada ya kusikilizwa kwa Shauri hilo, Mahakama ya Wilaya Mbarali ilitoa amri ya utaifishaji wa ng'ombe hao, mnada uliendeshwa na Dalali wa Mahakama na kiasi cha **Shillingi 8,095,000** kilipatikana. Ng'ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 213,026.31**;

ix. Tarehe 13/12/2022, ng'ombe **138** walikutwa katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha katika eneo la Ukangi. wamiliki wa ng'ombe hawakupatikana. Shauri Namba **26/22** lilifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya Mbarali. Katika shauri hili, Mahakama pia ilitoa amri ya utaifishaji wa ng'ombe. Ng'ombe hao

kuuzwa kwa mnada na kiasi cha **Shillingi 51,470,000** kilipatikana. Katika mnada huu, ng'ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 372,971**;

x. Tarehe 13/12/2022, ng'ombe **60** walikutwa katika eneo la Mwima ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Wamiliki wa ng'ombe hawakupatikana. Shauri Namba **27/22** lilifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya Mbarali. Mahakama ilitoa amri ya utaifishaji wa ng'ombe hao. Kiasi cha Shilingi **21,002,000** kilipatikana baada ya kuuzwa. Katika mnada huo, ng'ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 350,033**;

xi. Tarehe 27/12/2022, ng'ombe **25** walikutwa katika eneo la Mwima ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Katika tukio hili, wamiliki wa ng'ombe hawakupatikana. Shauri Namba **02/2023** lilifunguliwa mahakamani ambapo Mahakama ya Wilaya Mbarali ilitoa amri ya utaifishaji wa ng'ombe ambao waliuzwa kwa mnada ulioendeshwa na Dalali wa Mahakama. Kiasi cha **Shillingi**

**4,970,000** kilipatikana na ng'ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 198,800.00**;

xii. Tarehe 31/1/2023, ng'ombe **135** walikutwa katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha katika eneo la Nyota Range Post. Wamiliki wa ng'ombe hawakupatikana. Shauri Namba **03/2023** lilifunguliwa mahakamani na Mahakama kutoa amri ya utaifishaji wa ng'ombe hao na mnada uliendeshwa na Dalali wa Mahakama. Kiasi cha **Shillingi 64,750,000** kilipatikana. Wastani wa ng'ombe mmoja aliuzwa kwa **479,629.62;**

xiii. Tarehe 6/02/2023, ng'ombe wengine **13** walikamatwa katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha katika eneo la Ikoga Wilaya ya Mbarali. Katika tukio hili pia wamiliki wa mifugo hawakupatikana. Shauri Namba **04/2023** lilifunguliwa mahakamani. Mahakama ilitoa amri ya utaifishaji na uuzwaji wa ng'ombe hao. Mnada uliendeshwa na Dalali wa Mahakama na kiasi cha **Shillingi 4,640,000.00** kilipatiakana. Katika mnada huu ng'ombe

mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 356,923.08**; na

xiv. Tarehe 6/02/2023, ng'ombe **90** na punda **6** walikamatwa katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha katika eneo la Ikoga Wilaya ya Mbarali na wamiliki wa mifugo hiyo hawakupatikana. Shauri Namba **05/2023** lilifunguliwa mahakamani. Mahakama ilitoa amri ya utaifishaji na uuzwaji wa mifugo hiyo na kiasi cha **Shillingi 32,434,000.00** kilipatiakana. Katika mnada huu mfugo mmoja uliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 337,854.17.**

**Picha 2.1: Baadhi ya Picha Mbalimbali za Mifugo na Mnada wa Mifugo Iliyokutwa katika Hifadhi ya Ruaha Mkoani Mbeya**





## 2.2. Mkoa wa Morogoro

Katika Mkoa wa Morogoro, jumla ya matukio mawili ya uingiaji wa mifugo hifadhini yaliripotiwa. Matukio hayo yalihusisha ng'ombe **690.** Kufuatia kukamatwa kwa ng'ombe hao, Mashauri Mawili yalifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya ya Morogoro ambapo Mahakama ilitoa amri ya utaifishaji wa ngombe wote **690.** Ng'ombe waliuzwa na jumla ya **Shilingi 190,700,000.00** zilipatikana.

Matukio ya ukamataji wa ng'ombe yalitokea katika Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere kama ifuatavyo:

i. Tarehe **24/12/2022**, ng'ombe **224** walikamatwa katika Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere katika eneo la Kimero Wilaya ya Morogoro. Wamiliki wa Ng'ombe walipatikana na kufikishwa Mahakama ya Wilaya ya Morogoro ambapo Shauri Namba **217/2022** lilifunguliwa. Watuhumiwa walipatikana na hatia na Mahakama kuwaadhibu kifungo cha mwaka mmoja (1) gerezani pia amri ya utaifishaji wa ng'ombe hao ilitolewa. Mnada uliendeshwa na Dalali wa Mahakama ambapo kiasi cha **Shillingi**

**67,200,000** kilipatikana. Ng'ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 292,173.91**; na

ii. Tarehe **17/01/2023,** ng'ombe **460** walikutwa katika Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere katika eneo la Kimero Wilaya ya Morogoro. Wamiliki wa Ng'ombe hawakupatikana. Shauri Namba **02/2023** lilifunguliwa mahakamani. Baada ya kusikiliza, Mahakama ilitoa amri ya utaifishaji na uuzwaji wa ng'ombe hao. Kiasi cha **Shillingi 123,500,000.00** kilipatiakana. Katika mnada huu ng'ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 268,478.26.**

**Picha 2.2: Picha za Ng'ombe Zilizokutwa katika Hifadhi ya Mwalimu Nyerere Mkoani Morogoro**



## 2.3. Mkoa wa Katavi

Katika Mkoa wa Katavi, jumla ya matukio matatu (**3)** ya uingiaji wa ng'ombe hifadhini yaliripotiwa yaliyohusisha ng'ombe **198.** Jumla ya mashauri matatu yalifunguliwa katika Mahakama za Wilaya ya Mlele na Mpanda, ambapo Mahakama zilikubali maombi ya Jamhuri ya kutaifisha na kuuza mifugo husika.

Baada ya mauzo, kiasi cha **Shilingi 108,908,000** zilipatikana. Matukio hayo ya ukamataji wa ng'ombe yalitokea katika Hifadhi ya Taifa ya Katavi kwa nyakati tofauti kama ifuatavyo;

i. Tarehe 29/1/2023, ng'ombe **32** walikamatwa katika Hifadhi ya Taifa ya Katavi. Wamiliki wa ng'ombe hawakupatikana na Shauri Namba **01/2023** lilifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya Mlele ambapo baada ya kusikiliza, Mahakama ilitoa amri ya utaifishaji wa ng'ombe hao. Mnada uliendeshwa na Dalali wa Mahakama na kiasi cha **Shillingi 11,685,000** kilipatikana. Ng'ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 365,156.25**;

ii. Tarehe 12/1/2023, ng'ombe **134** walikamatwa katika Hifadhi ya Taifa ya Katavi, wamiliki wa ng'ombe hawakupatikana. Shauri Namba **02/2023** lilifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya Mlele ambapo baada ya kusikiliza, Mahakama ilitoa amri ya utaifishaji wa ng'ombe hao. Mnada uliendeshwa na Dalali wa Mahakama na , kiasi cha

**Shillingi 82,265,000** kilipatikana. Ng'ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 613,917.91**; na

iii. Tarehe **3/1/2023,** ng'ombe **32** walikamatwa katika Hifadhi ya Taifa ya Katavi. Wamiliki wa ng'ombe hawakupatikana. Shauri Namba **03/2023** lilifunguliwa katika Mahakama ya Mpanda. Mahakama ilikubali maombi ya Jamhuri na kutoa amri ya utaifishaji wa ng'ombe hao. Kiasi cha **Shillingi Tsh14,958,000** kilipatikana baada ya ng'ombe hao kuuzwa kwa mnada ulioendeshwa na Dalali wa Mahakama. Ng'ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 467,437.50**.

**Picha 2.3: Baadhi ya Picha za Ng'ombe Zilizokutwa katika Hifadhi ya Katavi Mkoani Katavi**





## 2.4. Mkoa wa Mara

Katika Mkoa wa Mara, jumla ya matukio **tisa (9)** ya uingiaji wa ng’ombe hifadhini yaliripotiwa yaliyohusisha ng’ombe **2,560**. Jumla ya mashauri tisa yalifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya ya Serengeti ya kuomba utaifishaji wa ng’ombe. Ng’ombe zote ziliamriwa kuuzwa na jumla ya kiasi cha **Shilingi 487,745,500** zilipatikana. Matukio hayo ya ukamataji wa ng’ombe yalitokea katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kwa nyakati tofauti kama ifuatavyo;

i. Tarehe **10/1/2023,** ng’ombe **300** walikutwa katika eneo la Warangi ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Wamiliki wa ng’ombe hawakupatikana. Shauri Namba **17/2023** lilifunguliwa mahakamani. Mahakama ilitoa amri ya utaifishaji wa ng’ombe hao. Kiasi cha **Shillingi 57,000,000** kilipatikana baada ya ng’ombe hao kuuzwa kwa Mnada ulioendeshwa na Dalali wa Mahakama. Ng’ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 190,000**;

ii. Tarehe **8/1/2023,** ng’ombe **663** walikutwa katika eneo la Miinuko ya Kofia ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Wamiliki wa

ng’ombe hawakupatikana. Shauri Namba **18/2023** lilifunguliwa mahakamani na Mahakama kutoa amri ya utaifishaji wa ng’ombe hao. Mnada uliendeshwa na Dalali wa Mahakama na kiasi cha **Shillingi 125,970,000** kilipatikana. Ng’ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 190,000**;

iii. Tarehe **8/1/2023**, ng’ombe **227** walikamatwa tena katika eneo la Miinuko ya Kofia ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Wamiliki wa ng’ombe hawakupatikana. Shauri Namba **19/2023** lilifunguliwa mahakamani na Mahakama kutoa amri ya utaifishaji wa ng’ombe hao. Mnada uliendeshwa na Dalali wa Mahakama na kiasi cha **Shillingi 58,885,500** kilipatikana. Ng’ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 259,000**;

iv. Tarehe **8/1/2023**, ng’ombe **19** walikutwa katika eneo la Machochwe ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Wamiliki wa ng’ombe hawakupatikana. Shauri Namba **20/2023** lilifunguliwa mahakamani na Mahakama kutoa amri ya utaifishaji wa ng’ombe hao. Mnada uliendeshwa na Dalali wa Mahakama na kiasi cha **Shillingi 3,610,000** kilipatikana.

Ng’ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 190,000**;

v. Tarehe **8/1/2023,** ng’ombe **540** walikutwa katika eneo la Machochwe ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Wamiliki wa ng’ombe hawakupatikana. Shauri Namba **21/2023** lilifunguliwa mahakamani na Mahakama kutoa amri ya utaifishaji wa ng’ombe hao. Kiasi cha **Shillingi 102,600,000** kilipatikana baada ya ng’ombe hao kuuzwa kwa Mnada ulioendeshwa na Dalali wa Mahakama. Ng’ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 190,000**;

vi. Tarehe **8/1/2023,** ng’ombe **23** walikamatwa tena katika eneo la Machochwe ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Wamiliki wa ng’ombe hawakupatikana. Shauri Namba **22/2023** lilifunguliwa mahakamani na Mahakama kutoa amri ya utaifishaji wa ng’ombe hao. Mnada uliendeshwa na Dalali wa Mahakama na kiasi cha **Shillingi 4,600,000** kilipatikana. Katika mnada huo ng’ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 200,000**;

vii. Tarehe **14/12/2022,** ng'ombe **294** walikutwa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti katika eneo la Machochwe. Wamiliki wa ng'ombe hawakupatikana. Shauri Namba **23/2022** lilifunguliwa mahakamani. Baada ya kusikiliza hoja za Jamhuri, Mahakama ilitoa amri ya utaifishaji wa ng'ombe hao. Ng'ombe wote waliuzwa kwa Mnada ulioendeshwa na Dalali wa Mahakama ambapo kiasi cha **Shillingi 48,420,000** kilipatikana. Ng'ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 164,693**;

viii. Tarehe **12/12/2022,** ng'ombe **11** walikutwa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti katika eneo la Machochwe. Wamiliki wa ng'ombe hawakupatikana. Shauri Namba **24/2022** lilifunguliwa mahakamani na Mahakama kutoa amri ya utaifishaji wa ng'ombe hao. Mnada uliendeshwa na Dalali wa Mahakama na kiasi cha **Shillingi 1,900,000** kilipatikana. Ng'ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 172,727.27**; na

ix. Tarehe **21/12/2022,** ng'ombe **483** walikutwa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti katika eneo Machochwe. Wamiliki wa ng'ombe

hawakupatikana. Jamhuri ilifungua Shauri Namba **25/2023** ikiomba, pamoja na mambo mengine, utaifishaji wa ng’ombe. Baada ya kusikiliza Mahakama ilitoa amri ya utaifishaji wa ng’ombe hao. Mnada uliendeshwa na Dalali wa Mahakama, kiasi cha **Shillingi 84,760,000** kilipatikana. ng’ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 175,000.**

**Picha 2.4: Baadhi ya Picha za Ng’ombe Zilizokutwa katika Hifadhi ya Serengeti Mkoani Mara**





## 2.5. Mkoa wa Pwani

Katika Mkoa wa Pwani kuliripotiwa tukio moja lililotokea tarehe **30/12/2022** ambapo ng'ombe **133** walikutwa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere katika eneo la Congo Ridge katika Wilaya ya Kisarawe. Wamiliki wa ng'ombe hawakupatikana. Shauri Namba **01/2023** lilifunguliwa mahakamani na Mahakama ilitoa amri ya utaifishaji wa ng'ombe hao. Kiasi cha **Shillingi 49,210,000** kilipatikana. Ng'ombe waliuzwa kwenye mnada ulioendeshwa na Dalali wa Mahakama. Ng'ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 370,000.**

## 2.6. Mkoa wa Manyara

Katika Mkoa wa Manyara, jumla ya matukio matatu ya uingiaji wa mifugo hifadhini yaliripotiwa yaliyohusisha ng'ombe **93,** mbuzi **13** na kondoo **54.** Jumla ya mashauri **matatu (3)** yalifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya ya Babati ya kuomba utaifishaji wa mifugo yote iliyoingia hifadhini. Mifugo yote iliamriwa kuuzwa na jumla kiasi **18,961,000.00** zilipatikana.

Matukio hayo ya ukamataji wa mifugo yalitokea katika Hifadhi ya Taifa ya Tarangire kwa nyakati tofauti kama ifuatavyo;

i. Tarehe **15/12/2022,** mbuzi **13** na kondoo **54** walikutwa katika eneo la Mswakini ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangire. Wamiliki wa mifugo hawakupatikana. Jamhuri ilifungua Shauri Namba **3/2023** katika Mahakama ya Wilaya Babati. Mahakama ilitoa amri ya utaifishaji wa mifugo hiyo na mnada wa uuzaji uliendeshwa na Dalali wa Mahakama. Kiasi cha **Shillingi 2,912,500** kilipatikana. Mfugo mmoja uliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 45,291.04**;

ii. Tarehe **17/12/2022**, ng'ombe **43** walikutwa katika Hifadhi ya Tarangire eneo la Chibi.

Wamiliki wa ng'ombe hawakupatikana. Shauri Namba **2/2023** lilifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya Babati. Mahakama ilitoa amri ya utaifishaji wa ng'ombe hao. Kiasi cha **Shillingi 6,853,500** kilipatikana baada ya ng'ombe kuuzwa kwa mnada ulioendeshwa na Dalali wa Mahakama. Ng'ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 159,383.72;** na

iii. Tarehe **14/01/2023,** ng'ombe **50** walikutwa katika eneo la Msitu wa George ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangire ambapo wamiliki wa ng'ombe walipatikana na kufikishwa Mahakama ya Wilaya ya Babati. Katika Shauri Namba **9/2023**. watuhumiwa walipatikana na hatia na Mahakama kuwadhibu kulipa faini ya **Shilingi 300,000** au kifungo cha miezi minne gerezani. Aidha, Mahakama ilitoa amri ya utaifishaji wa ng'ombe hao. Mnada uliendeshwa na Dalali wa Mahakama ambapo kiasi cha **Shillingi 9,195,000.00** kilipatikana. Katika mnada huu, ng'ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 183,900.00.**

## 2.7. Mkoa wa Tabora

Katika Mkoa wa Tabora, kuliripotiwa tukio moja**,** lililotokea tarehe **4/1/2023** ambapo ng'ombe **319** walikutwa katika Hifadhi ya Taifa ya Kigosi katika eneo la Mingungani Wilaya ya Kaliua. Wamiliki wa ng'ombe walipatikana na kufikishwa mahakamani na kisha kutiwa hatiani katika Shauri Namba **06/2023.** Mahakama ilitoa amri ya utaifishaji wa ng'ombe hao. Mnada uliendeshwa na Dalali wa Mahakama na kiasi cha **Shillingi 113,853,000,00** kilipatikana. Ng'ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 356,905.96.**

## 2.8. Mkoa wa Simiyu

Katika Mkoa wa Simiyu, jumla ya matukio sita ya uingiaji wa mifugo hifadhini yaliripotiwa yaliyohusisha ng'ombe **371**, mbuzi **4** na kondoo **5.** Jumla ya Mashauri Sita yalifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya ya Bariadi. Jamhuri iliomba amri ya utaifishaji wa mifugo hiyo. Mifugo yote ilitaifishwa kwa amri ya Mahakama na kuuzwa na Dalali wa Mahakama. Jumla ya kiasi cha **Shilingi 60,427,900.00** kilipatikana**.**

Matukio hayo ya ukamataji wa mifugo yalitokea katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kwa nyakati tofauti kama ifuatavyo;

i. Tarehe **22/11/2022**, katika matukio mawili, ng’ombe **57** walikutwa katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti (Tukio moja lilihusisha ng’ombe 22 na tukio lingine lilihusisha ng’ombe 35 ambao waliokutwa katika sehemu tofauti). Wamiliki wa mifugo hawakupatikana. Mashauri Namba **12/2022** na **13/2022** yalifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya Bariadi ambayo ilitoa amri ya utaifishaji wa mifugo hiyo. Mnada uliendeshwa na Dalali wa Mahakama na kiasi cha **Shillingi 7,000,000.00** kilipatikana. Katika mnada huo ng’ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 122,807.02**;

ii. Tarehe **15/12/2022,** katika matukio mawili**,** ng’ombe **146** walikutwa katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti (Tukio moja lilihusisha ng’ombe 84 na tukio lingine lilihusisha ng’ombe 62 ambao waliokutwa katika sehemu tofauti). Wamiliki wa mifugo hawakupatikana. Mashauri Namba **92/2022** na **01/2023** yalifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya Bariadi ambayo ilitoa amri ya utaifishaji wa mifugo hiyo. Kiasi cha **Shillingi 27,200,000.00** kilipatikana

kutokana na kuuzwa kwa mifugo katika mnada wa hadhara uliosimamiwa na Dalali wa Mahakama. Ng'ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 186,301.37**;

iii. Tarehe **5/1/ 2023,** jumla ya ng'ombe **94,** mbuzi **4** na kondoo **5** walikutwa katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, wamiliki wa mifugo hawakupatikana. Shauri Namba **5/2023** lilifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya Bariadi. Mahakama ilitoa amri ya utaifishaji wa mifugo hiyo ambapo iliuzwa kwa mnada uliondeshwa na Dalali wa Mahakama. Kiasi cha **Shillingi 16,947,300.00** kilipatikana. Katika mnada huo mfugo mmoja uliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 164,536.89;** na

iv. Tarehe 22/1/2023, ng'ombe 65 walikutwa katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na wamiliki wa mifugo hawakupatikana. Jamhuri ilifungua Shauri Namba **06/2023** katika Mahakama ya Wilaya Bariadi ikiomba amri ya Mahakama kutaifisha mifugo hiyo. Mahakama ilitoa amri ya utaifishaji na uuzaji wa mifugo hiyo kwa kusimamiwa na Dalali wa Mahakama ambapo kiasi cha **Shillingi 9,280,600.00**

kilipatikana. Ng’ombe mmoja aliuzwa kwa wastani wa **Shillingi 142,778.46.**

# 3. UTARATIBU WA UKAMATAJI NA MAUZO

## 3.1. Taratibu za Ukamataji

Taratibu za ukamataji zinafanywa na Askari wa Hifadhi husika. Baada ya mifugo kukamatwa taarifa zinaripotiwa katika Vituo vya Polisi vya jirani na hifadhi kisha taarifa zilitangazwa katika vijiji husika ili kutafuta wamiliki wa mifugo iliyokamatwa. Kwa wale wamiliki wanaopatikana au kujitokeza hufikishwa mahakamani kwa makosa ya kuingiza mifugo hifadhini bila kibali. Kwa upande wa wamiliki waliokosekana maombi huwasilishwa mahakamani ya kuomba mifugo kutaifishwa na kuuzwa kwa njia ya mnada wa hadhara kwa kutumia Dalali wa Mahakama husika. Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (OTM) hufungua mashauri mahakamani baada ya upelelezi kukamilika na majalada yenye taarifa muhimu kuhusiana na matukio hayo kuwasilishwa Ofisi za Mashtaka katika maeneo husika.

### 3.2. Taratibu za Mauzo

Mauzo hufanyika kwa uwazi kwa kushirikisha Kamati za Ulinzi na Usalama kwenye baadhi ya maeneo. Mifugo yote huuzwa kwa njia ya mnada wa hadhara kufuatia amri ya Mahakama na Dalali wa Mahakama aliyeteuliwa ndio wanahusika na kutekeleza amri ya Mahakama kwa kufuata taratibu za mnada.

Baada ya uuzaji, Dalali wa Mahakama anarejesha taarifa mahakamani na kuwasilisha gharama alizozitumia katika mnada ambapo gharama alizotumia zinaondolewa kutoka kwenye kiasi cha jumla kilichopatikana na kiasi kilichobaki kinawekwa katika **Akaunti ya Serikali No**. **52010101511 - Forfeited Assets and Revenue Collection Account (NMB Bank).**

**Picha 3.1: Zoezi la Mnada wa Ng'ombe Likiendelea**



## 4. MAFANIKIO

Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika zoezi hili ni Pamoja na;

i. Utaratibu wa kufungua kesi mahakamani na Mahakama kutoa amri ya utaifishaji wa mifugo umepunguza makosa ya uingizaji wa mifugo hifadhini;

ii. Kupungua kwa matukio ya kuingiza mifugo Hifadhini kumeimarisha uhifadhi pamoja na kulinda ekolojia na kuzuia magonjwa kwa

wanyama. Aidha, matukio ya wanyama pori kama vile Simba na Chui kuuawa na wafugaji yamepungua;

iii. Kupungua kwa vitendo vya ujangili hifadhini ambao ulikuwa ukitendwa kutumia njia ya wafugaji; na

iv. Utaratibu wa kufungua kesi mahakamani umepunguza changamoto zilizokuwa zinatokana na malalamiko ya hatua za Ufifishaji (Compounding of Offences) zilizokuwa zinachukuliwa na Mamlaka za Uhifadhi.

## 5. CHANGAMOTO.

Licha ya mafanikio kupatikana katika zoezi la kufungua mashauri mahakamani na kuomba mifugo iliyoingia hifadhini kutaifishwa na kuuzwa kwa mnada, bado zipo changamoto katika hatua hizi ambazo zinapaswa kupatiwa ufumbuzi wa haraka. Changamoto hizo ni pamoja na;

i. Umbali wa vituo na miundombinu duni ya barabara ambapo mifugo iliyokamatwa huhifadhiwa kunasababisha kutokufika wateja kwa idadi ya kutosha hivyo kuathili bei kutokana na ushindani hafifu katika

minada inayoendeshwa na kuibua malalamiko kutoka kwa wafugaji na na Waheshimiwa Wabunge kuwa minada ya aina hii ni nyenzo ya watu wachache kujipatia vipato visivyokuwa halali;

ii. Wateja walionunua mifugo kuvamiwa na wafugaji na kuporwa mifugo waliyoinunua katika minada imejenga hofu kwa wanunuzi kwenda kwenye minada kwa kuhofia kunyanganywa mifugo baada ya kununuliwa hivyo kuathiri ushindani wa bei;

iii. Kesi kuchelewa kusikilizwa na kutolewa maamuzi mapema kunasababisha mifugo kukaa muda mrefu bila kuhudumiwa ipasavyo na hivyo kusababisha ng’ombe kudhoofu jambo ambalo linaathiri bei na wakati mwingine kupelekea ng’ombe kuuzwa kwa makundi kwa bei ndogo;

iv. Wahifadhi wanao tunza na kulinda mifugo iliyokamatwa kuvamiwa na wanyama wakali kwenye hifadhi. Aidha, kazi ya kuchunga mifugo kupunguza nguvu kazi kwa Wahifadhi kwakuwa huacha shughuli yao ya msingi ya uhifadhi na kutumia muda mwingi kuchunga mifugo iliyokamatwa hifadhini; na

v. Wafugaji wanapotaifishiwa mifugo hutoa malalamiko kwa Waheshimiwa Wabunge wa maeneo husika kuonyesha kuonewa hata kama Sheria zimefuatwa na hivyo kupelekea mgongano wa kimaslahi kati ya Serikali na wananchi.

## 6. MAPENDEKEZO

Kufuatia uzoefu uliopatikana na changamoto zilizojitokeza tunashauri mambo yafuatayo;

i. Sheria ya Uhifadhi Sura 282 ifanyiwe marekebisho hususani katika vifungu vya 20A(1)(I) na 28(1)(i) vinavyohusiana na ufifirishaji wa makossa (compounding of offences) ili kuweka;

   a. Ulinganifu katika kiasi kinachopaswa kutozwa wakati wa ufifirishaji wa makosa;

   b. Kubainisha kama kiasi kitakachototozwa kitahusu mfugo mmoja au kundi zima la mifugo lililoingia hifadhini; na

   c. Kuongeza kiasi cha adhabu kwa njia ya ufifishaji wa makosa kwakuwa kiwango kinachotozwa sasa hakijafanikiwa kuhofisha wahalifu kutotenda kosa hilo.

Ufifirishaji sahihi utasaidia kuokoa muda wa kufungua kesi mahakamani.

ii. Kuweka utaratibu wa kisheria utakaolazimu mashauri ya uingizaji wa mifugo hifadhini kusikilizwa mapema na kwa haraka ili kuepusha gharama za utunzaji na uhifadhi wa mifugo iliyokamatwa;

iii. Kuwekwa kwa alama za kudumu katika mipaka ya Hifadhi;

iv. Uhamasishaji wa ufugaji wa kisasa badala ya makundi makubwa ya mifugo yanayozidi uwezo wa malisho;

v. Wanakijiji wanaopakana na hifadhi kupewa elimu kuhusiana na Sheria za Uhifadhi na umuhimu wa uhifadhi pamoja na uhifadhi wa mazingira; na

vi. Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya kushirikishwa kikamilifu pale hatua za kisheria zinapochuliwa kwa wafugaji wanaoingiza mifugo hifadhini. Hii itapunguza malalamiko ya uonevu na rushwa kwa wasimamizi wa Sheria za Uhifadhi.

## 7. HITIMISHO

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka itaendelea kutekeleza majukumu ya kimashtaka kwa kuzingatia Sheria na taratibu zilizopo. Hata hivyo, uzoefu unaonesha kuwa, hatua zozote zinazochukuliwa na Serikali kulinda Hifadhi za Taifa zinaongeza chuki baina ya wafugaji na wahifadhi au wasimamizi wote wa sheria, hata kama haki imetendeka. Aidha, yapo malalamiko ya mipaka katik a hifadhi zetu ambayo kama hayatatatuliwa tutaendelea kupata malalamiko ya wananchi kuhisi hawatendewi haki kwa mifugo yao kuamini imekamatwa nje ya mipaka ya Hifadhi. Ni rai yetu kuwa Mamlaka za uhifadhi zianishe mipaka yote ya hifadhi kwa alama za kudumu na za wazi.

Kutokana na changamoto za kisheria zilizojitokeza, ni rai ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kuwa sheria zote zinazohusika kulinda maeneo yote yaliyohifadhiwa zipitiwe upya ili kuondoa mgongano hususani katika eneo la adhabu na ufifirishaji wa makosa.

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka itaendelea kushirikiana na Taasisi zinazohusika na uhifadhi ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za kisheria kwa watuhumiwa wanaokinzana na Sheria za

Uhifadhi na kutoa mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria husika pale itakapobidi kufanya hivyo.

**Sylvester Anthony Mwakitalu**

**MKURUGENZI WA MASHTAKA**